


## 7. Mbinu mchanganiko za kuangamiza

### kwekwe

Mbinu mbili au zaidi kati ya zile zilizotajwa hutumiwa sambamba kuangamiza kwekwe na huwa na matokeo yenye manufaa ya kimazingira na kifedha.

### KUMBUKA

Ili kupata mazao ya juu na yaliyo bora, kuzingatia wakati na kutoharibu fedha na vipengele muhimu kuzingatia katika mbinu hizi zote za kuzuia kwekwe.



Mapata mazuri ya mahindi



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.kari.org

### Mtayarishaji:

Mwangi, H.W.

### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

### Mkuu wa Kituo,

KARI-Kabete

S.L.P. 14733-00800, Nairobi

Simu: (020)4444144

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 8 / 2008

**Shilingi 20 za Kenya**

**Jinsi ya kudhibiti  
kwekwe ili kuwa  
na mavuno mengi**



## Utangulizi

Hali ya kushindana baina ya mahindi na kwekwe inaweza kuleta gharama kwa shamba nzima kulingana na maswala kadhaa ya kwekwe.

Maswala haya ni kama:

- i) Aina ya kwekwe kama vile:
  - Nyasi au majani mapana
  - Inyokua pekee au vimelea
  - Uhai wa kwekwe (za Mwaka mmoja, za miaka miwili au za miaki zaidi ya miwili.
- ii) Kiwango cha wingi wa kwekwe.
- iii) Nyakati za kwekwe kushindana na mahindi.

Swala lolote liwalo, wakati wa kupalilia na hali ya kwekwe ni lazima liangaliwe ili kuepukana na uharibifu wa mazao kutokana na ukosefu wa maadili ya afya na unyevu.

## Mbinu za kukinga kwekwe

Mbinu za kupigana na athari za kwekwe zilizopo ni kama:

### I. Utayutarishaji wa ardhi:

Hili ndilo jambo la kwanza na muhimu katika kuangamiza kwekwe. Huanzia na kuondoa vichaka vichaka baada ya kulima na plau na kuchimbua. Katika kuchimbua hata kulima kwa kiwango cha chini, dawa ya kuangamiza kwekwe hutwiwa.



Ardhi ilivyotayarishwa vizuri

### 2. Kulima kwekwe kwa mkono

Hii hufanyawa kwa kutumia vifaa kama vile jembe, visu au plau. Kupalilia mara mbili kati ya wiki ya pili na ya saba baada ya mimea kuchipuka kunatosha kulingana na mazingira ya hali ya hanga.

Hii inafaa:

- Kupalilia mara ya kwanza baada ya wiki mbili au tatu
- Kupalilia mara ya pili baada ya wiki sita au saba baada ya kuchipuka.

### 3. Mimea ya kufunikia ardhi ambazo mimea imechanyanywa

Mimea ya jamii ya kunde hukuzwa pamoja na mahindi, ili kunyonga kwekwe. Mifano ni kama kunde, *mucuna*, *cloraria* and *dolichos*.

- Mimea hii inafaa kuwa na uwezo wa kumea kwa kasi na yenye majani mengi ili kufunika ardhi kabla ya kwekwe kutokea.



Mahindi yamekuzwa na mimea mingine

### 4. Ardhi iliyotengwa

Mimea iliyotajwa hapo awali inaweza kukuzwa peke yake katika ardhi iliyotengwa ili kuzuia kwekwe kumea na kunyonga ile inayomea.

### 5. Kufunikia ardhi na matawi na majani ya mimea

Haya ni masalio ya mimea ambayo hutumiwa kufunikia nafasi zilizoko katikati ya mimea. Mbinu hii ni nadra kwa sababu ya ukosefu wa majani na matawi ya kufunikia na kuliwa na mchwa.

### 6. Kuzuia kwekwe kwa kutumia kemikali za kuua kwekwe

Hizi ni kemikali ambazo huaa kwekwe. Zinatengenezwa katika aina ya unga au majimaji.

Baadhi ya dawa hizi huaa kwekwe kabla ya kumea au kutokea na zinaitwa *pre-emergence herbicides*. Hizi hutwiwa juu ya mchanga kavu baada ya kupanda na huaa kwekwe inapotokea.

Dawa zingine huaa kwekwe zinapokutana nazo na huitwa *post-emergence herbicides*. Hizi hutumika katika mashamba madogo madogo.

Ili kutumia dawa hizi ifaavyo, ujuzi na vifaa mwafaka ni muhimu.



Dawa zinazoua kwekwe wakati kwekwe zimemea